



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. NA. HMD/S.20/44/119

17/11/2021.

## TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

KWA MUJIBU WA KIBALI CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KIKAO CHA TAREHE 15/11/2021 MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WENYE SIFA AMBAO NI RAIA WA TANZANIA KUOMBA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA KAMA IFUATAVYO:-

1. MADEREVA (20)

(a) SIFA.

- (i) AWE RAIA WA TANZANIA.
- (ii) AWE NA ELIMU YA KIDATO CHA IV.
- (iii) AWE NA LESENI YA UDEREVA KATIKA DARAJA E AU C YA UENDESHAJI MAGARI NA AMEENDESHA GARI KWA KIPINDI CHA MWAKA MMOJA (1) BILA KUSABABISHA AJALI.
- (iv) AWE AMEHUDHURIA MAFUNZO YA UENDESHAJI WA MAGARI (BASIC DRIVING COURSE) YANAYOTOLEWA NA CHUO CHA UFUNDI STADI (VETA) AU CHUO CHOCHOTE KINACHOTAMBULIWA NA SERIKALI.
- (v) MWENYE CHETI CHA MAJARIBIO YA UFUNDI DARAJA LA II WATAFIKIRIWA KWANZA.

## KAZI NA MAJUKUMU.

- (i) KUKAGUA GARI KABLA NA BAADA YA SAFARI ILIKUBAINI HALI YA USALAMA WA GARI.
- (ii) KUPELEKA WATUMISHI MAENEO MBALIMBALI YA SAFARI.
- (iii) KUFANYA MATENGENEZO MADOGO YA GARI.
- (iv) KUKUSANYA NA KUSAMBAZA NYARAKA MBALIMBALI
- (v) KUJAZA NA KUTUNZA TAARIFA ZA SAFARI ZOTE KATIKA DAFTARI LA SAFARI
- (vi) KUFANYA USAFI WA GARI
- (vii) KUFANYA KAZI NYINGINE KADRI ATAKAVYOELEKEZWA NA MSIMAMIZI WAKE.

MSHAHARA: TGS B YAANI 430,000 NA KUENDELEA.


### MAMBO YA JUMLA YA KUZINGATIA.

1. WAOMBAJI WOTE WAVE NA UMRI USIOZIDI MIAKA 45 NA USIOPUNGUA MIAKA 18.
2. AJIRA HII NI YA MKATABA WA MWAKA MMOJA NA MASHARTI MENGINE YA AJIRA HII YATAKUWA KATIKA MKATABA WA AJIRA.
3. WAOMBAJI WOTE WAAMBATANISHE VIVULI VYA VYETI VYAO KWENYE BARUA ZA MAOMBI, PIA WAANDIKE NAMBA ZAO ZA SIMU.
4. BARUA ZIBANDIKWE PICHA MBILI ZA (STAMP SIZE)
5. WATAKAOTIMIZA MASHARTI YALIYOTAJWA WATATAARIFIWA TAREHE YA USAILI KUPITIA SIMU ZAO.

6. MAOMBI YOTE YATUMWE KWA ANUANI IFUATAYO.

MKURUGENZIWAJIJI  
HALMASHAURIYAJIJI LA DODOMA  
S.L.P 1249,  
DODOMA.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 1 DISEMBA, 2021 SAA  
9.30 ALASIRI NA MAOMBI YATAKAYO WASILISHWA BAADA YA  
MUDA HUO HAYATAPOKELEWA.



JOSEPH C. MAFURU  
MKURUGENZI WA JIJI  
DODOMA,

